Pg1 The Guardian Agosti 15/2025



# PM orders completion of BRT-2

Page 3

Agosti 15/2025 Pg 3

The Guardian
www.ippmedia.com

# PM wants speed in BRT-2 works to ease traffic congestion in Dar

**By Guardian Reporter**

PRIME Minister Kassim Majaliwa has instructed managers of the second phase of Bus Rapid Transit (BRT-2) project to work round the clock to complete all remaining sections to enable commuter services to begin and ease traffic congestion in Dar es Salaam.

Majaliwa made the directive on Wednesday evening after inspecting the new buses for BRT-2 project and its infrastructure, including the main bus terminals at Mbagala Rangi Tatu and Gerezani. He also visited the construction site for a specialized gas filling station for the buses, located at Mbagala Rangi Tatu terminal.


"We want this project to start serving residents of Dar es Salaam. This project will increase efficiency of public transport in the city and provide modern, safe and fast services to the public," he said.

Majaliwa also instructed management of Mofat Mohammad Kassim, the service provider, to expedite the release of 99 buses currently at the port to ensure services start on time.

CamScanner

Mwananchi Agosti 15/2025 Pg 11

# Sauti ya wananchi



BARUA YA MSOMAJI

## Ya Kimara yasije Mbagala

**Mhariri,**

Napenda kuchukua nafasi hii kupongeza hatua ya kuanzishwa kwa huduma ya mabasi ya mwendokasi (BRT) katika njia ya Mbagala, hatua ambayo ni ya kihistoria na yenye matarajio makubwa kwa wananchi wa maeneo haya.

Ni dhahiri kuwa mradi huu utapunguza msongamano wa magari, kurahisisha usafiri wa abiria, na kuongeza ufanisi wa muda wa safari.

Hata hivyo, mafanikio ya mradi huu yatategemea kwa kiasi kikubwa namna unavyosimamiwa. Ukisimamiwa vizuri manufaa yake yataonekana lakini ikiwa kinyume na hivyo tutayaona yanayoendelea kwenye barabara ya Morogoro.

Huko tunashuhudia kila uchwao watu wakilalamikia adha ya usafiri wa mwendokasi unaosababishwa na uchache wa magari na wakati mwingine mabasi mengi kutofanya kazi kwa sababu ya ubovu. Hatutamani haya yatokee kwenye mradi wa Mbagala.

Hilo linanifanya nisisitize kuna umuhimu kuhakikisha ratiba za mabasi zinafuatwa kwa wakati, vyombo vinatunzwa vizuri, na huduma inakuwa ya kiwango cha juu ili kuondoa kero ambazo mara nyingi hujitokeza katika miradi mikubwa ya umma.

Aidha, ulinzi wa abiria na nidhamu ya watumishi lazima izingatiwe ili kuwajengea wananchi imani na hamasa ya kutumia usafiri huu.

Vilevile, wahusika wanapaswa kuhakikisha kuwa bei ya nauli inabaki kuwa nafuu na unafanyika ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kuzuia mianya ya upotevu wa mapato au ubadhirifu wa rasilimali.

Mradi huu ukiendeshwa kwa weledi, utakuwa mfano bora wa miradi ya usafiri wa kisasa nchini, na kuleta matokeo chanya kiuchumi na kijamii.

Ni matarajio yangu kuwa mamlaka husika zitalinda na kuendeleza mradi huu ili uwe chachu ya maendeleo na siyo kero mpya kwa wakazi wa Mbagala na maeneo jirani.

**Msomaji**

Mwananchi Agosti 15/2025 Pg 11



Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Wilaya ya Ileje, Kisbert Kapondo (kulia) akizungumza na abiria waliokuwa kwenye basi akiwapa elimu kuhusu madhara ya kujazana kupita kiasi katika vyombo vya moto na umuhimu wa kuzingatia sheria na kanuni za usalama barabarani, ili kupunguza ajali katika barabara ya Ileje-Mbeya Vijiji mkoani Songwe. **Picha na Issa Mwadangala**

Mwananchi Agosti 15/2025 Pg 22

# Afya ya akili na tabia zinavyosababisha ajali



DK SHITA SAMWEL

**PIRAMIDI YA AFYA**

Maswali na majibu piga na sms kwa simu: 0763-296752

Uwepo wa matatizo ya afya ya akili hasa yaliyojificha ikiwamo sonona au mfadhaiko, unaweza kuwa chanzo cha kusababisha ajali nyingi katika jamii.

Lakini pia waathirika wa ajali hizo wanaweza kupata matatizo ya akili ikiwamo hofu na kuganda kwa tukio linaloumiza akilini.

Matatizo ya afya ya akili kama vile ulevi na matumizi mabaya ya dawa za kulevya yanaweza kuongeza hatari ya ajali kutokana na uamuzi mbovu, tabia hatarishi na kushindwa kudhibiti mfadhaiko.

Kupata ajali mbaya kunaweza kusababisha hali kama vile wasiwasi na mfadhaiko wa akili baada ya tukio la zamani.

Hali hizi za afya ya akili huathiri uwezo wa mtu wa kuendesha gari kwa usalama au kufanya kazi kwa usahihi kama inavyotakiwa.

Mtu mwenye hali ya kuyumba kwa fikra kiuamuzi na tabia hatarishi na kubadilika hisia anaweza kusababisha uamuzi wa haraka haraka na hivyo kuongeza uwezekano wa kuendesha gari bila uangalifu.

Utumiaji mbaya wa pombe na dawa za kulevya, ambazo mara nyingi huhusishwa na matatizo ya afya ya akili, zinaweza kuharibu kwa kiasi kikubwa utendaji wa utambuzi, uratibu hivyo kufanya watu binafsi kukabiliwa na ajali. Hali kama vile mfadhaiko na wasiwasi zinaweza kusababisha usumbufu wa kulala na kuongezeka kwa viwango vya mfadhaiko, na kusababisha uchovu na kupungua kwa umakini ambavyo vinaweza kuwa hatari wakati wa kuendesha gari au kuendesha mashine.

Baadhi ya hali za afya ya akili zinaweza kuathiri utendaji wa utambuzi kama vile kumbukumbu, umakini na ufanyaji uamuzi. Hii hufanya iwe vigumu kuitikia ipasavyo katika hali za ajali au dharura. Lakini pia kupata ajali kunaweza kuathiri afya ya akili hivyo kumweka mwathirika katika hatari ya kusababisha ajali kama atakuwa ni dereva au mwendesha mitambo.



Ajali zinaweza kuwa matukio ya kuhuzunisha sana, na kusababisha kuwa na mgando wa matukio ya kuumiza, wasiwasi na mfadhaiko huku watu binafsi wakijitahidi kukabiliana na matokeo ya kimwili na ya kihisia.

Waathiriwa wa ajali wanaweza kukuza hofu na wasiwasi mwingi kuhusu kuendesha gari au kuwa ndani ya gari, hivyo kufanya iwe vigumu kuendelea na shughuli za kawaida ikiwamo kuendesha.

Majeraha ya ubongo yanayotokana na ajali yanaweza kusababisha uharibifu wa kudumu wa utambuzi, kuathiri kumbukumbu, umakini na ujuzi wa kutatua matatizo au mambo ya kila siku.

Uzoefu wa ajali mbaya ikiwa ni pamoja na majeraha ya kimwili, hofu, na hasara inayoweza kutokea kama vile kufariki au kuumia, unaweza kusababisha mfadhaiko mkubwa wa kihisia ikiwa ni pamoja na kukereketwa, kuchanganyikiwa, hasira na hofu.

Ili kijikinga na ajali zinazotokana matatizo ya kiakili, ni muhimu waendesha vyombo vya moto hasa vya abiria na magari makubwa kufanyiwa uchunguzi wa kina wa afya.

**USULI**

**Matatizo ya afya ya akili kama vile ulevi na matumizi mabaya ya dawa za kulevya yanaweza kuongeza hatari ya ajali kutokana na uamuzi mbovu, tabia hatarishi na kushindwa kudhibiti mfadhaiko.**

UTEKELEZAJI

# Majaliwa ashusha kibano wasimamizi Mwendokasi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amewaagiza waendeshaji awamu ya pili ya mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT-2) kuhakikisha wanafanya kazi usiku na mchana ili kukamilisha maeneo yaliyobaki yatakayowezesha mradi huo kuanza kutoa huduma ndani ya muda mfupi.

Alielekeza hayo juzi wakati alipokagua mabasi mapya kwa ajili ya awamu ya pili ya mradi wa mabasi yaendayo haraka (BRT-2) pamoja na miundombinu ikiwamo kituo kikuu cha mabasi hayo cha Mbagala Rangi Tatu na kituo cha gerezani, jijini Dar es Salaam.

Waziri Mkuu pia alitembelea ujenzi wa kituo maalum cha kujazia gesi kwa ajili ya mabasi hayo, kinachojengwa katika kituo cha Mbagala Rangi Tatu.

"Tunataka mradi huu uanze kutoa huduma kwa Watanzania hasa wakazi wa Dar es Salaam, mradi huu utaongeza ufanisi wa usafiri wa umma katika jiji la Dar es Salaam na kutoa huduma ya kisasa, salama na ya haraka kwa wananchi," alisema.

Majaliwa alimwagiza Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya utoaji huduma ya Usafiri ya Mofat, Mohammad Kassim kuhakikisha anakamilisha haraka taratibu za utoaji mabasi 99 yaliyoko bandarini ili kuwezesha huduma hiyo kuanza kwa wakati.

Alisema serikali inataka kuona katika awamu ya pili ya mradi wa BRT, tiketi za usafiri kupitia mabasi hayo zinakuwa za kielektoniki badala ya tiketi za karatasi kama ilivyokuwa awali. "Tukifanya hivi itatusaidia kumonitor kiasi cha fedha kinachokusanywa."



Aidha, Majaliwa alitoa wito kwa Watanzania kuchangamkia fursa za ajira zitakazotokana na mradi huo ukiwamo udereva.

"Nendeni mkasome masuala ya udereva kupitia Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), mradi huu utahitaji idadi kubwa ya madereva wenye ujuzi," alisema.

Akizungumza baada ya kukagua kituo cha kujaza gesi mabasi hayo kilichoko kwenye kituo kikuu cha Mbagala Rangi Tatu, Majaliwa aliagiza kampuni ya nishati inayotekeleza mradi huo kuhakikisha wanakamilisha usimikaj mitambo ili waanze kutoa hu duma.

Katika ziara hiyo, Wazir Mkuu aliambatana na Wazir wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), William Lukuvi, Naibu Waziri Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Zainab Katimba, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Dk. Jim Yonazi pamoja na watendaji wengine wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Wakala ya Mabasi Yaendayo Haraka (DART) na uongozi wa NIT.



Mkandarasi akiendelea na ujenzi wa ukuta wa zege wa kuzuia mmomonyoko wa ardhi pembeni mwa barabara ya Morogoro, eneo la Kimara Kona, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam jana, ikiwa ni sehemu ya upanuzi wa barabara hiyo inayotarajiwa kuwa na njia sita. **PICHA: SABATO KASIKA**

CamScanner

AJALI BARABARANI: *Nipashe Agosti 15/2025 Pg 8*

# Wananchi wapewa elimu maalum ya kudhibiti uzembe wa madereva

**Na Issa Mwadangala,** ILEJE

KATIKA jitihada za kuimarisha usalama barabarani na kupunguza ajali zinazosababishwa na uzembe wa baadhi ya watumiaji wa vyombo vya moto, Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Wilaya ya Ileje, Mrakibu Msaidizi wa Polisi (ASP) Kisbert Kapondo, ametoa elimu maalum kwa wananchi wa eneo la Iwiji, barabara ya Ileje-Mbeya, mkoani Songwe.

Akizungumza jana mbele ya mamia ya wananchi na madereva wa vyombo vya moto, ASP Kapondo, alisisitiza umuhimu wa kufuata sheria na kanuni za usalama barabarani, akieleza kuwa uzembe wa baadhi ya madereva umekuwa chanzo kikuu cha ajali nyingi ambazo husababisha vifo na ulemavu usiotarajiwa.

Katika hotuba yake, ASP Kapondo alieleza kwa msisitizo athari za tabia ya baadhi ya madereva wa magari ya mizigo kubeba abiria, akisema kuwa magari hayo hayajatengewa kusafirisha watu na hivyo ni hatari kwa maisha ya abiria wanaopanda.

Alitolea mfano wafanyakazi wa migodini wanaosafirishwa kwa namna hiyo, akieleza kuwa ni wajibu wa madereva kuhakikisha wanatii sheria kwa usalama wa wote.

"Ni marufuku kubeba abiria kwenye magari ya mizigo. Haya magari hayana hadhi ya kubeba watu, na kufanya hivyo ni sawa na kuhatarisha maisha ya wasio na hatia," alisema ASP Kapondo.

Aidha, alikemea vikali tabia ya madereva wa pikipiki, maarufu bodaboda, kuendesha vyombo vyao wakiwa wamezidisha abiria kinyume cha sheria, akisema hali hiyo imechangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la ajali nchini.

"Acheni kuendesha magari mabovu na pikipiki bila leseni halali. Hakikisheni vyombo vya moto vina viakisi mwanga (reflectors) ili kuepusha ajali hasa nyakati za usiku na mvua," aliongeza.

Mbali na kutoa elimu, ASP Kapondo pia aliongoza ukaguzi wa vyombo vya moto ambapo jumla ya makosa 39 ya usalama barabarani yalibainika na hatua za kisheria kuchukuliwa ikiwamo kulipishwa faini.

Kati ya makosa hayo, pikipiki 11 zilihusishwa, jambo linalodhihirisha kiwango kikubwa cha ukiukwaji sheria miongoni mwa waendesha bodaboda.

ASP Kapondo aliwaasa abiria na watumiaji wengine wa barabara kutoshiriki kwa njia yoyote katika uvunjaji sheria kwa kukaa kimya au kuvumilia vitendo vinavyohatarisha usalama wao.

Alisisitiza kuwa usalama wa barabarani ni jukumu la kila mmoja na kila mwananchi anapaswa kuwa sehemu ya mabadiliko kwa kutoa taarifa kuhusu madereva wazembe.

"Ukiona dereva anakiuka sheria, sema. Toa taarifa. Ukikubali kupanda gari au pikipiki isiyo salama, na wewe ni sehemu ya tatizo. Tuwe wazalendo kwa kulinda maisha yetu na ya wenzetu," alihimiza.

Akihitimisha, ASP Kapondo aliwataka watumiaji wote wa barabara kutambua kuwa utii wa sheria ni nguzo muhimu katika kulinda maisha, kukuza uchumi na kuimarisha maendeleo ya taifa.

CamScanner

P96





Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo (wa tatu kulia) akikabidhi cheti cha uwakala wa kutoa leseni za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Saccos ya Chama cha Ushirika cha Maofisa Usafirishaji wa Pikipiki Mkoa wa Dar es Salaam (MAUPIDA), Athanas Kitime (wa nne kushoto) katika hafla iliyofanyika Dar es Salaam juzi. Wengine ni Mwenyekiti wa Shirikisho la Bodaboda, Said Chenja (wa tatu kushoto) na Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara Latra, Johansen Kahatano. (wa pili kulia). (Na Mpigapicha Wetu).






*ILALA District Commissioner, Edward Mpogolo (third right) hands over a Land Transport Regulatory Authority (LATRA) licence to the Chairman of Maupida SACCOS, Atunas Kitime during a ceremony held in Dar es Salaam on Wednesday. Also present is the Director of Road Transport Regulation at LATRA, DCP Johansen Kahatano (second right) along with other leaders. (Photo by a Correspondent)*

CamScanner